

Pambazuko

Toleo Namba 057

Jumatatu Januari 15-21, 2024

TB Joshua aumbuliwa na binti yake

Tuhuma za 'Nabii' TB Joshua; za kutesa na kuwanyanyasa kingono, wasichana ndani ya kanisa lake, zimeibuliwa na binti yake, baada ya kuwa mmoja wa waathirika...

Soma Uk. 16



Jicho la Tai Chalamila sasa umekua, jitambue, thibitisha **Uk. 5**

Maaskofu 500 Wamgomea Papa... UK. 6

UGANDA	RWANDA	KENYA	DR CONGO
Makali kukosa ufadhili yaanza kuuma Uk. 10	Kagame asikitika uamuzi wa Burundi Uk. 12	Mizozo yafukuta Azimio la Umoja Uk. 13	Kibarua kizito kwa Rais Tshisekedi Uk. 15

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Pongezi Rais Samia kuwamulika Dart

VYOMBO vya habari vina nafasi adhimu ya kuchochea na kuleta mabadiliko; yawe mazuri na hata wakati mwingine, mabaya, kutegemea na mukhtadha wa habari, makala na pengine picha, zinazosambazwa na vyombo hivyo.

Vyombo hivyo; magazeti, redio, televisheni, na sasa mitandao ya kijamii, vina nguvu kubwa, endapo vitaaminika zaidi kutokana na kufanya kazi zake kwa weledi, uaminifu, kutoumiza wengine na kikubwa zaidi, kujali jamii.

Kwa vyombo vya habari ambavyo vinasimamia misingi ya taaluma ya kupasha habari, nguvu yake inabaki kuheshimika na kuaminika kwamba ni mhimili wa nne – usiokuwa rasmi, wa dola, ukiachana na mihimili mingine; Bunge, Mahakama na Serikali.

Kwa mukhtadha huu, sisi Pambazuko tunampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kwa kuchukua haraka hatua za kufanya mabadiliko kwenye uongozi wa wakala wa mabasi yaendayo haraka (Dart) kwa kumuweka pembeni Mkurugenzi Mtendaji, Dkt. Edwin Mhede na kumteua Dkt. Athuman Kihamia.

Tunampongeza Rais Samia kwa sababu ni wiki moja tu zimepita tangu safu ya Hoja Yangu – iliyoko ukurasa wa tisa, ndani ya gazeti hili la Pambazuko, ihoji ujasiri wa Mkurugenzi wa Dart (aliyeondolewa sasa), kuacha mabasi 70 yakiegewa kwa madai ya ubovu, huku wananchi wa Jiji la Dar es Salaam wakihangaika asubuhi na jioni – kwa shida ya

usafiri.

Inashangaza kwamba, licha ya fedha za umma kuwekwa kwenye mradi huo, mabasi yake yanaachwa tu “yakioza” eti kwa kuwa na changamoto ndogondogo za kiufundi ambazo zinaweza kutatuliwa bila kuhitaji “mzungu” kurekebisha.

Oktoba 12, mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Albert Chalamila aliwapa wiki mbili wakala hao, kuhakikisha mabasi 70 mabovu yaliyosimama, yanarudi barabarani kuendelea na kazi, ili kuondoa adha ya usafiri kwa wakazi wa jiji hilo kubwa na mahsusii la kibiashara.

Maagizo hayo ya Chalamila yalitokana na malalamiko ya wananchi jijini humo ambao wanapata adha kubwa ya usafiri wa kwenda na kurejea kazini na majumbani kila siku kama yalivyoibuliwa na baadhi ya vyombo vya habari.

Hata hivyo, mpaka Januari Mosi, 2024 Pambazuko tulihoji ujasiri wa baadhi ya watendaji serikalini akiwemo mkurugenzi huyo wa Dart, aliyeacha mabasi 70 yakiharibika bila hofu, huku akijua mradi huo umegharimu fedha nyingi – nyingine zikiwa ni mikopo, kutoka taasisi za fedha za kimataifa. Hadi tarehe hii, hakukuwa na utekelezaji wowote wa maagizo ya Chalamila.

Sisi Pambazuko tunaona uamuzi huu umekuja kwa wakati, na ishara ya utawala bora, hivyo tunachukua fursa hii kumpongeza Rais Samia kwa hatua hii ya ujasiri yenye lengo la kuboresha uwajibikaji wa Dart.

WALINZI WETU...

Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) akipita kwa mbwembwe kuonesha mavazi, silaha na vifaa vingine vinavyotumiwa na makomandoo wa jeshi hilo. Hiyo ilikuwa Ijumaa - Januari 12, 2024 wakati wa sherehe za maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Amani, Zanzibar. (Picha ya Ikulu).



Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



Amini Mungu atafanya yote, lakini hatarajii kwamba utakalia jembe usubiri mashimo ya kupanda mbegu yajichimbe yenyewe kimiujiza
- Mchungaji Emmanuel Mgaya (Masanja Mkandamisaji).

Tangazo

Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

Mhariri Mkuu,
Oktoba, 2023

Changia Pambazuko liendelee

WAJUMBE wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufuraha kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakituma fedha, muda, ujuzi na rasilimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokuwa zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukaza Kiwahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeviza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yamewekwa wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majaraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kumarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kusuzwa, lakini hasi kubaliana na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapata kuchangia maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sawa ya "asante" kutoka kwetu.

Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263

Ukituma mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandika: **Pambazuko Gazeti**. Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.

Lipa kwa Simu

Lipa kwa kuscana

Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI

Chalamila sasa umekua, jitambue, thibitisha

Na Igo AI

TAI ni muumini mkubwa mno wa mawazo, mitazamo na misimamo ya aliyekuwa kiongozi wa kwanza wa Tanganyika huru – Mwalimu Julius Kambarage Burito Nyerere.

Ifahamike kuwa Tanganyika ilibadilishwa jina na kuitwa Tanzania, baada ya kuwepo muungano wa nchi mbili; Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964.

Ni kutokana na imani hiyo ya Tai kwa Mwalimu Nyerere (sasa marehemu), hajaacha kusoma maandishi ya mwana huyo wa Afrika ambaye, pamoja na kuwa kaburini, bado heshima yake inamea.

Jana Tai alionekana yuko bize mno akichakura karatasi moja baada ya nyingine kwenye ‘makabati’ yake ya vitabu, hakumwambia lolote mwandishi wake, ambaye mara zote humpa majukumu ya namna hiyo.

Baada ya muda mfupi, Tai akapiga ngumi ukutani, huku akishusha pumzi kwa nguvu; “haaaaaah!”

Kulikoni boshi? Akauliza mwandishi wa Tai. Akamjibu kwamba alikuwa anatafuta wapi aliweka andiko na kauli ya Mwalimu Nyerere kuhusu msimamo wake juu ya maandamano ya vyama vya upinzani.

Tai akamuita mwandishi wake na kumweleza kitu cha kuandika juu ya kauli ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila kuhusu maandamano yaliyoitishwa na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Aikaeli Mbowe.

Mbowe wiki iliyopita aliueleza umma wa Tanzania na dunia kwamba Januari 24, mwaka huu – Siku ya Jumatano, anahimzia kuwepo kwa maandamano ya amani ambayo yatakuwa na ujumbe wa kuitaka serikali kujali zaidi wananchi kwa kuhakikisha miswada kadhaa ya sheria; hasa za uchaguzi, inaondolewa na kupelekwa upya bungeni. Kwamba ifanyiwe marekebisho.



*Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,
Albert Chalamila*

Pia Mbowe anaitaka serikali kujali wananchi kwa kuhakikisha gharama za maisha; hasa kupanda kiholela kwa bei za vyakula, kunadhibitiwa.

Sasa bhana! Tai alipoipata kauli ya Mwalimu Nyerere, akasikika akisonya; nyvyuuuu! Huku akifoka –“ Mwalimu Nyerere, mwenye Tanzania yake, anaruhusu maandamano, nani mwingine wa kuzuia?”

Tai akaendelea; “hivi unajua Mwalimu alikasirika sana kusikia serikali eti inamzuia Agostino Lyatonga Mrema kuandamana na kubebwa kama jeneza, wakati wa vuguvugu la uchaguzi wa mwaka 1995!”

Tai akaomba aletewe Katiba na Tanzania, akaipeka na kuisoma na baadaye akang’aka; “mbona katiba nayo inaruhusu maandamano, hawa wanaozuia ni kina nani? Hivi watu wakitaka kuelezea kero zao wanazuiwa?”

Tai akadai amesikia Chalamila anaelekeza majeshi kuingia barabarani siku hiyohiyo ya maandamano, akasema; “huyu mkuu wa mkoa anatumia janjajanja kuzuia maandamno ya wananchi bila sababu yoyote kwa jina la majeshi kufanya usafi.”

Akasema; kumbe bado Chalamila anajidogosha, ndiyo maana aliwekwa pembeni, anajiona hakui. Hebu aache sasa. Amekua!

•*Wasiliana na mwandishi wa Tai
kwa namba: 0754 020 880.*

Habari

Maaskofu 500 Afrika wamgomea Papa

Na Mwandishi WETU

Umoja wa Mabaraza ya Maaskofu wa Afrika na Madagascar (Secam), kwa kauli moja umepinga uamuzi wa Papa Francis juu ya “baraka zisizo za kiliturujia” kwa wapenzi wa jinsia moja, ambazo zilipendekezwa katika Tamko la Vatican, litwalo “Fiducia Supplicans.”

Tangu kuchapishwa kwake, Desemba 18, mwaka jana - 2023, tamko la “Fiducia Supplicans” limekuwa likikoselewa mara kadhaa na maaskofu mbalimbali na mabaraza ya maaskofu duniani, kwa madai kwamba linapingana na “hazina ya imani” Katoliki kuhusu ndoa ya jadi ya Kikristo, ambayo inafundisha wahusika kwenye ndoa ni; mwanamume na mwanamke.

Sasa, wakiwa wanajibu tamko hilo la Vatican, maaskofu zaidi ya 500 wa Afrika wametoa taarifa ya pamoja yenye upinzani ambapo wanasema; “hakutakuwa na baraka kwa wapenzi wa jinsia moja, (wapenzi mahunta na wapenzi wenye jinsia pindu) katika makanisa ya Katoliki katika ardhi ya Afrika.”

Barua ya Januari 11, 2024 iliyoandikwa kwa Papa Francis, na nakala yake kuonwa na Pambazuko, imesainiwa na Kadinali Fridolin Ambongo, Rais wa Secam ikiwa na kichwa kisemacho; hakuna baraka kwa wapenzi wa jinsia moja katika Bara la Afrika.

Ambongo anasema barua hiyo ni muhtasari wa maoni ya maaskofu wote wa Afrika, ambayo yalitumwa kwake kujibu tamko la Papa Francis alilolitoa kwao kuhusu mashoga.

Katika barua hiyo, Ambongo anasema kwamba ingawa maaskofu wa Afrika “wamethibitisha kwa nguvu zao zote ushirika wao wenye afya na Papa Francis,” bado “wanaamini kwamba “baraka zisizo za liturujia” zilizopendekezwa katika Tamko la ‘Fiducia Supplicans’ haziwezi



Papa Francis

kutolewa katika Afrika.”

Barua hiyo ya Secam inataja sababu kumi za upinzani wa jumla wa maaskofu wa Afrika dhidi ya mapendekezo ya “baraka zisizo za kiliturujia” kwa miungano ya wapenzi wa jinsia moja; kwamba baraka wa mashoga ni kinyume na mapenzi wa Mungu na kwa hiyo haiwezi kupokea baraka za Kanisa.”

Maaskofu hao pia wanadai kwamba, vitendo vya kujamiiana vya hiari kwa njia ya ulawiti, kama wafanyavyo baaadhi ya wapenzi wa jinsia moja, vimefitinika na kuwa ni kinyume cha sheria ya maadili asilia kuhusu ndoa na familia.

Viongozi hao wa Katoliki Afrika pia wanaeleza kuwepo kwa utata wa Tamko la Papa na kwamba linazua dhana potofu na machafuko katika akili za waumini wengi waaminifu, watu waliojiweka wakfu, na hata wachungaji, na imeamsha hisia kali na kujaribu kuvuruga amani ndani ya Kanisa Katoliki kwa mambo ambayo yanakengeusha Kanisa na kulifanya liachane na vipaumbele vyake vya sasa.

Rais wa kwanza wa Secam alikuwa Mtanzania, Kadinali Laurean Rugambwa (sasa marehemu) – mwaka 1969.



Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com

Mezani kwa Chahali

Chalamila na kipyenga cha Chadema

Na Evarist Chahali

JUZI, Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasi na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, alitangaza kuwa chama hicho kitafanya maandamano ya amani katika Jiji la Dar es Salaam, Jumatano ya Januari 24, mwaka huu, 2024.

Lakini kabla mjadala kuhusu tamko hilo la Mbowe haujaanza, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila akatangaza kuwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na majeshi mengine ya usalama, yatafanya usafi kwa siku mbili mfululizo kuanzia Januari 23 hadi 24, 2024.

Hakika, hakuhitaji kuwa na ufahamu mkubwa kubaini kuwa tangazo la Chalamila limelenga kuzuia maandamano hayo. Kwamba Jeshi la Polisi litapata sababu nyingine ya kudai kuwa maandamano hayo ya Chadema yataingilia shughuli ya usafi wa jiji hilo kubwa la kibiashara.

Kabla ya kujadili tangazo la Chalamila, tutupie jicho tamko la Mbowe kuhusu maandamano hayo. Alieleza kuwa lengo la maandamano ya amani ni kuishinikiza serikali kutopuza maoni ya wananchi na kada mbalimbali, kuhusu masuala ya uchaguzi.

Baada ya kusikia tamko hilo, nilionelea vyema kupata maoni ya wadau mbalimbali kwenye baadhi ya mitandao ya kijamii kuhusu maandamano hayo.

Niliuliza maswali kadhaa.

Je “intelijensi ya Jeshi la Polisi” itaruhusu maandamano hayo?

Yakiruhusiwa, je, wananchi watajitokeza kwenye maandamano hayo?

Yasiporuhusiwa, je, Chadema watafanya maandamano hayo kwa



*Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,
Albert Chalamila*

nguvu?

Yakiruhusiwa au la, lakini yakafanyika, je, yatafikia malengo kusudiwa?

Japo Jeshi la Polisi halijatoa tamko lolote hadi wakati naandika makala haya, uzoefu unaweza kusaidia kuhitimisha kuwa jeshi hilo litakataa kutoa kibali kwa Chadema, kwa sababu zilezile za kawaida ambazo hazina tija kuzirudia hapa.

Lakini sasa, Chalamila amewapatia kisingizio kingine cha kupiga marufuku maandamano hayo, ambapo yayumkinika kuhisi kuwa jeshi hilo litadaia kuwa maandamano hayo yataathiri shughuli za usafi wa jiji zitakazofanyika kwa siku mbili mfululizo.

Ukweli ni kwamba shughuli hizo mbili; maandamano na usafi wa jiji – zinaweza kufanyika pasina hofu yoyote ya kuathiri nyingine, lakini ni wazi kuwa kinachotafutwa ni kisingizio cha kuzuia maandamano hayo.

Wadau wengi waliojadili tamko la Mbowe walionesha shaka kama wananchi watakojitokeza kuandamana endapo maandamano hayo yataruhusiwa na Jeshi la Polisi.

Baadhi yao walidai kuwa Chadema wamekuwa mahiri kuitisha maandamano ambayo hata viongozi wake hawajitokezi

Habari

Wakulima ufuta bado wasotea 'jasho lao'

Na Rashid MTAGALUKA

MGGORO kati ya wakulima wa ufuta na Chama cha Ushirika cha Msingi Nanjirinji 'A' - wilayani Kilwa, Lindi ni aibu.

Wanaoangukia kwenye aibu hiyo ni viongozi wa Wilaya ya Kilwa kwa upande wa kwanza, na Mkoa wa Lindi kwa ujumla wake, kwa kushindwa kuutatua kwa kipindi cha miaka miwili sasa.

Hatua ya viongozi kushindwa kutatua mgogoro huo uliogeuka kero kwa wananchi hao, na hasa kwa wakulima wa ufuta, kutolipwa malipo yao halali ya msimu wa mwaka 2022/2023 hadi sasa, siyo afya katika nchi inayoongozwa na rais anayejali na kuthamini utu wa Watanzania.

Ikiwa mkulima amepeleka ufuta wake gulioni na kupokewa na maofisa wa chama cha Ushirika Nanjirinji 'A' tangu Julai 2, 2022 kwa mfumo wa stakabadhi ghalani, na mpaka leo hajalipwa, viongozi wanasubiri nini kuingilia kati kutatua jambo hili?

Miongoni mwa wakulima waliozungumza na Pambazuko kutoka Nanjirinji, Kilwa ni pamoja na Rehema Christopher Mbila ambaye aliuza kilo 4,200 za ufuta kwenye chama hicho cha ushirika tangu Julai 02, 2022 na kupewa stakabadhi namba 964806 iliyosainiwa na karani Kindamba Kinongo, mpaka leo mwanamama huyo anahemea malipo yake.

Kupitia kadhia hii, kaka yake, Bakari Abdallah Imamu aliyesimamia mauzo ya zao hilo kutoka shamba hadi ghalani, anasimulia adha na manyanyaso anayokumbana nayo kwa miaka miwili sasa, akifuatilia malipo ya ufuta wa dada yake huyo bila mafanikio.

"Mimi nimelazimika kufuatilia malipo ya ufuta wa dada yangu hadi mahakama ya wilaya ya Kilwa Masoko na ikaamuliwa nilipwe fedha za kilo 4,200



Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack

sawa na shilingi milioni 13 na elfu 83, kama zinavyoonesha kwenye stakabadhi, lakini mpaka leo naambiwa malipo yapo kwenye process", alisema Imamu huku akimuonesha mwandishi nakala ya stakabadhi hiyo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack amekiri kulifahamu sakata hilo, ingawa hajawahi kumuona mlalamikaji na kwamba kutokana na madai ya ubadhirifu wa viongozi wa chama hicho, aliamuru kisimamishe shughuli zake za ununuzi wa mazao toka mwaka 2022.

"Najua Nanjirinji kuna wakulima ambao hawakulipwa hadi leo wanadai, na (hivyo) tukafunga chama kwa kuwa pia kulikuwa na tuhuma kubwa za ubadhirifu," ameongeza mkuu huyo wa mkoa.

Swali wanalojiuliza wengi ni ipi hatima ya wakulima wale wa ufuta wa Nanjirinji kuhusu malipo yao ya msimu wa 2022/2023 ambayo bila shaka walitarajia kulipa madeni yakiwemo viuatilifu walivyokopa wakati wa msimu wa kilimo huku chama kilichokopa mazao kikiwa korokoroni kwa amri ya mkuu huyo wa mkoa kutokana na upotevu wa zaidi ya tani 15 za ufuta?



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Pombe kali, vipodozi visiwe mtaji kwa Bima

Na Rashid Mtagaluka

NI kweli Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote wa mwaka 2022, umesainiwa na Rais Samia Suluhu Hassan na kuwa sheria kufuatia kutangazwa kwenye gazeti la serikali Desemba Mosi, mwaka jana.

Itakumbukwa kuwa Novemba 2022, Bunge lilipitisha muswada huo ambao pamoja na mambo mengine, umeainisha vyanzo mbalimbali vya mapato vitakavyotumika kupata fedha za kuhudumia Bima ya Afya kwa Wote.

Baada ya muswada huo kutiwa saini, Waziri wa Afya, Ummu Mwalimu alimshukuru Rais Samia kwa namna alivyoonesha kujali afya za wananchi wake, hususan wale wenye kipato cha chini.

Kisha Waziri Ummu akataja vyanzo vya mapato kuwa ni pamoja na ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vikali, bidhaa za vipodozi na kodi za michezo ya kubahatisha (kamari).

Vyanzo vingine kwa mujibu wa Waziri Ummu ni fedha zitakazotengwa na Bunge, mapato yatokanayo na uwekezaji wa mfuko, zawadi na misaada kutoka kwa wadau mbalimbali.

Uamuzi huo ni mzuri, ingawa wasiwasi wangu upo hapo kwenye pombe kali, vipodozi na kodi kutoka kwenye michezo ya kubahatisha kuwa vyanzo vyetu vya kutusaidia kupata fedha za kuhudumia Bima ya Afya kwa Wote.

Hivi inakuwaje serikali itegemeo vipaumbele vya kupata fedha za Bima ya Afya kwa Wote kwa kuweka rehani maisha ya watu haohao kwa kubariki matumizi ya vipodozi?

Mara ngapi tunasikia wataalamu wa afya kutoka wizara hiyo anayoongoza Waziri Ummu wakieleza aina zaidi ya 800



Waziri wa Afya, Ummu Mwalimu

tofauti za vipodozi ambavyo vingi kati yake ni hatari kwa ngozi ya binadamu?

Na ukitazama kiwango cha ufukara na urahibu wanaopata vijana wetu - kutwa kushinda kwenye mashine za madubwi na 'kuchana mikeka,' wakitaraji kutajirika, unagundua kama nchi, tunaelekea kusiko.

Tuchukue mfano mdogo wa Afrika Kusini, ambako kwa mujibu wa kitengo cha utafiti wa kitabibu nchini humo, kati ya mwaka 2003/2004 walikuwa wakikusanya mabilioni ya Rand kwa mwaka kupitia kodi ya pombe kali tu.

Lakini, matokeo yake serikali ikajikuta inaingia hasara baada ya kutumia zaidi ya makusanyo – mara saba kwa mwaka, kuhudumia watu walioathirika na ajali zilizosababishwa na unywaji wa pombe hizo zilizobarikiwa kwa lengo la kuongeza mapato ya kodi.

Hivyo basi, ushauri wangu kwa serikali, pamoja na mpango huo mzuri ijkite katika vyanzo vingine visivyokuwa hivi ili kuepuka kile kinachoweza kutafsiriwa kama 'kusukia ukambaa jikoni', maana zitakapokusanywa hizo fedha, kwa upande mwingine hatutakuwa na watu wa kuwahudumia tena!

•*Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu namba 0784 438 546. Barua pepe: mtagaluka@gmail.com*

Uganda

Makali kukosa ufadhili yaanza kuuma

Na Mwandishi WETU

UCHUMI wa Uganda, huenda ukakabiliwa na ugumu wa kuimarika zaidi kutokana na bajeti ya mwaka 2024/25, 'kufinywa.'

Maeneo mengi yaliyozoeleka kupata mgawanyo mkubwa wa fedha kwa miaka mingi iliyopita, sasa bajeti zake zinabanwa.

Hali hiyo inatokana na Uganda kukosa ufadhili kutoka nchi tajiri; hasa za Magharibi; Marekani, Canada, Uingereza na taasisi za fedha za kimataifa kwa kuwa nchi hiyo inarahamisha ushoga.

Mwishoni mwa wiki, Wizara ya Fedha imeieleza Kamati ya Bunge ya Bajeti kuwa msaada kutoka kwa nchi wahisani a mashirika ya kimataifa, unatarajiwa kupungua zaidi, kutoka dola za Marekani 732,963,975 mwaka 2023/24 hadi dola 7,627,464.02 pekee katika bajeti ijayo ya 2024/25.

Kukosekana kwa bajeti hiyo kutaathiri, kwa kiasi kikubwa shughuli za maendeleo, hasa katika sekta za afya, elimu na miundombinu.

Jane Aceng, ambaye ni Waziri wa Afya, ameonesha wasiwasi wake katika kufikia malengo katika baadhi ya maeneo ya sekta anayoiongoza kwa kuwa yatapokea bajeti finyu, hivyo kukwamisha matarajio.

Waziri huyo anasema kuwa ufadhili wa katika sekta ya afya unatarajiwa kushuka kwa hadi kufikia asilimia 49.

Hata hivyo, kama ambavyo imekuwa ikielezwa na seriali, waziri huyo naye amekataa kuhusisha kupungua kwa ufadhili na kuanza kutumika kwa sheria ya kupambana na mapenzi ya jinsia moja ya Mei 2023.

"Najua katika mawazo yenu, mnafikiri ni sheria ya kupinga mapenzi ya jinsia moja ndiyo chanzo, lakini sivyo," Waziri wa Afya, Jane Aceng aliambia kamati ya bunge.

"Ufadhili umekuwa ukishuka na



Rais wa Uganda - Yoweri Museveni

nimekuwa nikiwasilisha hili kwa sababu wafadhili hawawezi kutuunga mkono milele. Kweli, hivi majuzi, tulisikitishwa pale Pepfar ilipotangaza kujitoka, kukawa na majadala mzito kwenye baraza lao la mawaziri, "ameongeza.

Bunge la Uganda lilipitisha marekebisho ya sheria ya Kupinga mapenzi ya jinsia moja Mei 2023 na Marekani ikatishia kuondoa ufadhili kwa Uganda kupitia Mpango wa Rais wa Kupambana na Ukimwa (Pepfar).

Vikwazo kutoka Marekani Hadi sasa, Marekani imeiondoa Uganda kwenye utaratibu wa kunufaika na mpango wa biashara wa Agoa, kuanzia Januari 2024, baada ya nchi hiyo kupitisha sheria dhidi ya mapenzi ya jinsia moja mwezi Mei mwaka uliopita.

Agoa ilizinduliwa mwaka wa 2000, na Marekani kwa nia ya kuruhusu kuingiza bidhaa za Afrika katika soko la Marekani bila kulipia ushuru.

Hii ilikuwa na nia ya kuinua nchi za Afrika kiuchumi huku zaidi ya bidhaa 1800 zikiwa katika orodha hiyo.

Lakini, sasa Marekani imeamua kuiondoa Uganda katika mkataba huo kuanzia Januari 2024 ikidai Uganda imekiuka haki za kibinadamu.

Uganda imekashifu Marekani ikionya hatua hiyo itawadhuru watu wachache, hasa wakulima waliokuwa wanategema kuuza bidhaa zao Marekani kupitia mfumo huo.

Ukiwa Bukoba...

Furahia *Neno* Freshi Juisi

Pata juisi (sharubati) ya matunda halisi iliyoandaliwa kwa usafi wa hali ya juu kwa kujali afya ya mteja.

Kunywa juisi ya:

Embe	Nanasi/pinacolada
Passion	Tende
Parachichi	Tikiti
Karoti	

Pia tunandaa juisi mchanganyiko maalum wa matunda ili kuondoa uchovu na magonjwa nyemelezi (detox) na pia smoothie.

Wasiliana nasi kwa namba hii:

0753949488



Rwanda

Kagame asikitika uamuzi wa Burundi

Na Mwandishi WETU

UAMUZI wa Serikali ya Burundi kuamua kufunga mpaka wake na Rwanda, umepokewa kwa masikitiko na Rais wa Rwanda, Paul Kagame.

Ofisi ya Rais Kagame, imeeleza kusikitishwa na uamuzi wa Burundi kwa maelezo kwamba kulikuwa bado na muda wa kujadili na kufikia muafaka wenye manufaa kwa nchi zote mbili.

Katika taarifa ya Rwanda ambayo imefikia Pambazuko mwishoni mwa wiki, nchi hiyo inaeleza kwamba haina nyaraka rasmi, ikiwamo barua kutoka Burundi inayoelezea uamuzi huo, ingawa vyombo vya habari, hasa mitandao ya kijamii, vinaeleza uamuzi huo.

“Serikali ya Rwanda imepata taarifa hiyo kupitia vyombo vya habari kuhusu uamuzi wa upande mmoja wa Serikali ya Burundi kufunga tena mipaka yake na Rwanda,” imesema taarifa ya Rwanda.

“Uamuzi huu wa bahati mbaya utazuia usafirishaji huru wa watu na bidhaa kati ya nchi hizo mbili, na unakiuka kanuni za ushirikiano wa kikanda na utangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki,” Rwanda imeongezea.

Hatua hii ya Burundi kufunga mipaka yake na nchi ya Rwanda, inakuja siku chache baada ya Rais wa Burundi Evariste Ndayishimiye kuishutumu Rwanda kwamba inawaunga mkono waasi wa Burundi wa Red-Tabara.

Desemba 30, mwaka jana – 2023, Rwanda ilipinga madai ya kusaidia waasi wa Burundi na kueleza kuwa “haina hata chembe ya kufanya uamuzi wa kusaidia waasi.” yalipojitokeza.

“Serikali ya Rwanda inakataa maoni ya Rais wa Burundi Evariste Ndayishimiye anayedai kuwa Rwanda inaunga mkono makundi ya waasi wenye silaha ya Burundi walioko mashariki mwa DRC,” alisema Yolande Makolo, msemaji wa



Rais Paul Kagame

Rwanda mapema wiki iliyopita.

Hii ni baada ya waasi hao kufanya shambulio katika eneo la mpakani mwa Burundi na DRC na kua raia wasiopungua 20.

Rais wa Burundi Ndayishimiye aliishutumu Rwanda kwa kuwaunga mkono waasi wa vuguvugu la Burundi la Red-Tabara lenye makao yake mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Rais Ndayishimiye ameilaumu Rwanda imeshindwa kutoa ushirikiano na kukataa kuikabidhi Burundi watu wanaotuhumiwa kuhusika katika jaribu la mapinduzi mwaka wa 2015 na ambao Serikali ya Burundi inadai wamekuwa wakipanga mashambulizi dhidi ya Burundi wakiwa na ngome yao mjini Kigali.

Rwanda tayari ina mvutano na jirani yake mwingine, DRC, ambapo DRC imekuwa iliilaumu kwa kuunga mkono kikundi cha waasi wa M23. Tuhuma ambazo Rwanda pia imekuwa ikizikana siku zote.

Uasi wa M23 ulianzishwa mwezi Aprili 2012, ukitokea kutoka kundi la waasi la Congress for the Defence of the People, kundi la waasi ambalo lilipigana na Serikali ya DRC kati ya mwaka 2006 na 2009.

Mizozo yafukuta Azimio la Umoja

Na Mwandishi WETU

SASA ni dhahiri kwamba mizozo, sinanekana kuelekea kuimarika na kukomaa ndani ya kambi kubwa siasa ya Azimio la Umoja.

Hatua hiyo inafuatia kile kinachoeleza na wanasiasa na wachambuzi wa siasa za Kenya kuwa ni “kutoaminiana” kati ya viongozi wakuu wa kambi hiyo.

Wiki iliyopita, Kalonzo Musyoka, kiongozi wa Chama cha Wiper, ndani ya umoja huo, uliomtoa jasho William Ruto, wakati wa kampeni na hata ushindi kwenye uchaguzo mkuu wa mwaka 2022.

Ruto alishinda nafasi ya urais, baada ya kutangazwa kidedea kwa kumbwaga Raila Odinga, kiongozi wa Azimio la Umoja.

Mzozo unaofuka moshi kwa sasa ni kubuniwa na hatimaye kuanza kutangazwa kuwepo kwa kile kinachoitwa “Vuguvugu la Kamwene.”

Inaeleza kuwa kuanza kwa vuguvugu hilo ndani ya Azimio la Umoja, hakuna baraka za viongozi wote wakuu, na hasa Kalonzo Musyoka, ambaye anadaiwa kueleza waziwazi kuwa “vuguvugu hilo halina maana.”

Januari 9, Jumanne iliyopita, Musyoka aliongeza kwa kueleza msimamo wake kuwa vuguvugu hilo ni “butu kisiasa,” na kuongeza kwamba halitakuwa na ufanisi wowote wa maana katika siasa za Kenya.

Vuguvugu hilo lilibuniwa mwishoni mwa mwaka jana na wanasiasa wa Azimio la Umoja kutoka ukanda wa Mlima Kenya, lengo lake likiwa “kupaza sauti na kupewa nafasi zaidi kwenye ngazi za uamuzi kwa wanachama wanaotoka eneo hilo.”

Baadhi ya waanzilishi wa vuguvug hilo ni pamoja na Kiongozi wa Narc-Kenya, Martha Karua, Katibu Mkuu wa Chama cha Jubilee, Jeremiah Kioni na aliyekuwa waziri wa Kilimo, ndani ya serikali ya Rais Uhuru Kenyatta.



Kalonzo Musyoka

Kwenye mahojiano na kituo kimoja cha televisheni, Musyoka alilitaja kundi hilo kama “lililojikita kwenye ukabila”.

“Vuguvugu hilo halitaenda mahali, kwani msukumo wake mkuu ni wa kikabila, sitaki kulizungumzia sana, kwani halitaenda mahali hata kidogo,” alisema Musyoka.

Kiongozi huyo alilitaja kundi hilo kuwa ni mwanzo wa kujimaliza kisiasa kwa wote watakaomua kujihusisha nalo.

Alisema kundi hilo linabeba dalili zote za kuwepo kwa ubinafsi na uroho wa wanasiasa kutaka madaraka.

Kauli hizi za Musyoka zimeonekana kumkera Karua, aliyeeleza “kushangazwa kwake na wasiwasi wa Musyoka kuhusu kuanzishwa kwa Kamwene”.

“Ni nini kinachomhofisha ndugu yangu (Kalonzo) kuhusu Kamwene, ambapo amekuwa akilipaka tope kundi hilo kila mara?” akashangaa Karua, kwenye ujumbe alioandika katika mtandao wa X (zamani Twitter) alioandika siku moja bada ya kauli ya Musyoka.

Kutokana na majibizano hayo, wadadisi wanayataja kama ishara za wazi kuhusu mzozo unaoendelea kutokata katika Azimio.

Wanaonya kuwa majibizano baina ya Musyoka na Karua hayafai kuchukuliwa kwa urahisi, ikizingatiwa wawili hao ni vigogo wakuu katika mrengho huo.

Hadi sasa, Raila Odinga hajazungua hadharani msimamo wake kuhusu vuguvugu hilo lililoanzishwa.

Tangazo



Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au

Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Kibarua kizito kwa Rais Tshisekedi

Na Mwandishi WETU

SIKU tano zijazo kutokea leo, Felix Tshisekedi, ataapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Kuapishwa kwa Tshisekedi kunafuatia ushindi wake katika uchaguzi mkuu wa nchi hiyo uliofanyika Desemba 20, mwaka jana, 2023.

Baadhi ya wagombea wenzake, walipinga ushindi wa Tshisekedi, hivyo kwenda mahakamani wakidai kukiukwa kwa baadhi ya taratibu na 'vurugu' amabzo zilimbema mpinzani wao.

Hata hivyo, Mahakama ya Katiba ya Congo imethibitisha Jumanne, Januari 9, kwamba ushindi wa rais anayemaliza muda wake, Tshisekedi ni halali. Alipata asilimia 73.47.

Tshisekedi (60), ambaye sasa ana uhakika wa kuishi likulu wa nchi hiyo kwa muhula wa pili, uongozi wake utaendelea kuwa na kazi ngumu, hasa ya kuwatumikia wananchi zaidi ya milioni 100, wengi wao wakiwa 'mafukara.'

Mbali ya kuhakikisha kwamba wananchi wa DRC wanakuwa na unafuu wa maisha, Tshisekedi anakabiliwa na jambo jingine kubwa; hali ya usalama wa nchi yake dhidi ya Rwanda.

Hata hivyo, yapo matumaini kwamba Tshisekedi ataendeleza mazungumzo na Rais wa Rwanda, Paul Kagame kuhusu suala la usalama na kuzidisha amani baina ya mataifa hayo.

DRC na Rwanda zimekuwa katika mvutano wenye kuashiria kutetereka kwa uhusiano, hali ambayo ilikuwa tete, kiasi cha kutishia amani.

DRC imekuwa ikiituhumu Rwanda kwamba inasaidia kundi la waasi wa M23, ambao wamekuwa wakivuruga amani na usalama wa Congo. Rwanda mara zote imekuwa ikikanusha tuhuma hizo.

Wakati wa kampeni za urais, Tshisekedi



Rais Ndayishimiye - Picha ya BBC

aliambia dunia kwamba, akichaguliwa tena atahakikisha anaishambulia Rwanda ili iache kusaidia waasi.

"Nitaitisha mkutano wa bunge ili kuniidhinisha kutangaza vita dhidi ya Rwanda," alisema, mbele ya umati wa wanaharakati katika eneo la Place Sainte-Thérèse mjini Kinshasa.

Mbali na masuala ya usalama wa mipaka ya DRC, Rais Tshisekedi pia ana kibarua kingine kizito kuhakikisha analeta utulivu wa ndani ya nchi hiyo, hasa ule wa kisiasa, kwani wapinzani wake wakubwa – aliogombea nao urais; Moïse Katumbi, Denis Mukwege na Martin Fayulu, huenda wakahakikisha "wanamsumbia" kiongozi huyo kwa kuwa wanadai hakushinda kihalali.

Moïse Katumbi, ambaye alishika nafasi ya pili, analaani malalamiko kadhaa ikiwa ni pamoja na "kuwepo kwa mashine za kupigia kura katika nyumba za watu binafsi" na kuahidi kutokubali matokeo haya, na kutoa wito wa "maandamano ya amani".

Serikali kupitia msemaji wake, Patrick Muyaya, tayari imeonya kuwa haitakubali maandamano yoyote ya mitaani.

Kwa upande wa kuimarisha uchumi wa DRC, Tshisekedi bado atakuwa na kazi kubwa ya kuhakikisha kuwa mfumuko wa bei unadhitiwa, kwani hivi sasa malalamiko ni makubwa mno kuhusu kupanda kwa gharama za maisha, hasa bei ya vyakula.

Uchunguzi

TB Joshua aumbuliwa na binti yake

Na Timu ya BBC

SHIRIKA la Utangazaji la Uingereza (BBC) limefanya uchunguzi wa muda mrefu kuhusu tuhuma za TB Joshua; kutesa waumini wake na kuwanyanyasa kingoni.

TB Joshua aliyekuwa na sifa kubwa duniani kwa kuiaminisha dunia kuwa “anatenda miujiza” – kwa Jina la Mungu, alifariki dunia mwaka 2021.

Kiongozi huyo tajiri na mwenye ukwasi mkubwa nchini Nigeria, hatimaye ameumbuliwa ‘maovu’ yake na binti yake ambaye naye ni miongoni mwa wafuasi walioteswa na kunyanyaswa.

Inaelezwa kuwa TB Joshua, alimfungia binti yake mwenyewe na kumtesa kwa miaka kadhaa kabla ya kumwacha bila makao ya uhakika katika mitaa ya Lagos, Nigeria.

“Baba yangu alikuwa na woga, hofu ya mara kwa mara. Aliogopa sana kwamba mtu angezungumza maovu yake, basi huo ndoyoungokuwa mwisho wake,” anasema binti huyo, Ajoke - mfichua ukweli wa kwanza kufikia BBC kuhusu unyanyasaji alioshuhudia katika kanisa la baba yake, Kanisa la Sinagogi la Mataifa Yote (Scoon).

TB Joshua, aliyefariki dunia akiwa na umri wa miaka 57, anatumwiwa kwa unyanyasaji na mateso yaliyoenea kwa takriban miaka 20.

Hivi sasa akiwa na umri wa miaka 27, Ajoke anayeishi mafichoni, huku akiwa ameacha kutumia jina lake la ukoo “Joshua.” – Kutokana na sababu kadhaa, jina lake jipya halijachapishwa.

Machache yanajulikana kuhusu mama mzazi wa Ajoke, ambaye aliaminika kuwa mmoja wa washirika wa TB Joshua. Ajoke anasema alilelewa na Evelyn, mjane wa Joshua, tangu akiwa msichana mdogo.

Hadi umri wa miaka saba, Ajoke anasema alikuwa na maisha ya furaha sana, akienda likizo na familia ya Joshua katika maeneo yenye starehe na gharama



TB-Joshua - Picha ya gaseti la DP

kubwa za “kujitanua” kama Dubai.

Lakini siku moja kila kitu kilibadilika. Alifukuzwa shule kwa kosa, na mwandishi mmoja wa habari wa eneo hilo aliandika makala akimtaja kama mtoto wa nje wa TB Joshua. Alitolewa shuleni na kupelekwa katika boma la Scoan huko Lagos.

“Nililazimishwa kuhamia kwenye chumba cha wanafunzi. Sikujitolea kuwa mfuasi. Nililazimishwa kujiunga na kanisa la baba yangu,” anasema.

Wanafunzi wengi, ndani na nje ya Nigeria, walikuwa wanapenda kujiunga na kanisa hilo, wakitengeneza kundi la wasomi wafuasi wa TB Joshua ambao waliojitolea kumtumikia TB Joshua.

Wanafunzi wengi wa kujitolea, hasa waliokuwa wanatoka Ulaya na Marekani, waliishi naye ndani ya viunga vya kanisa.

Waliishi chini sheria kali; miongoni ikiwa ni marufuku kulala kwa zaidi ya nne kwa wakati mmoja, kupigwa marufuku kutumia simu zao wenyewe au kupata barua pepe zao za binafsi, na kulazimishwa kumwita TB Joshua “Daddy (baba)”.

“Wanafunzi walikuwa wamepewa mafunzo ya itikadi kali na walikuwa wawezeshaji wa madhila katika kanisa hilo. Kila mtu alikuwa akiigiza tu kwa kufuata amri - kama zombi. Hakuna aliyekuwa akihoji chochote,” anasema.

Akiwa mtoto tu, Ajoke hangefuata

Uchunguzi

TB Joshua aumbuliwa na binti yake

Inatoka Uk. 16

sheria kama wanafunzi wengine: alikataa kusimama wakati mchungaji alipolingia chumbani na kuasi amri kali za kulala.

Unyanyasaji ulivyoanza

Alipofika umri wa miaka saba, anakumbuka alipigwa kwa sababu ya kukojoa kitanda na kisha kulazimishwa kuzunguka eneo la nyumba akiwa amevalishwa kibao shingoni yake kilichokuwa na maandishi haya; "Mimi hukojoa kitandani."

"Ujumbe kuhusu Ajoke ulikuwa kwamba alikuwa na pepo wabaya sana ambao walihitaji kufukuzwa," anasema mwanafunzi mmoja wa zamani wa kike aliyekuwa rafiki wa binti huyo wa TB Joshua.

Baadaye binti huyo alihamishiwa kwenye mabweni yaliyomo ndani ya eneo la kanisa katika kitongoji cha Ikotun huko Lagos.

Kuhamishwa kwa Ajoke, kulimaanisha kwamba alikuwa ametengwa.

"Alikuwa, kama, aliyeitwa kondoo mweusi wa familia," anasema Rae, kutoka Uingereza, ambaye kwa miaka 12 aliishi kanisani kwa TB Joshua akiwa mfuasi kindakindaki. Kama wanafunzi wengi wa zamani waliohojiwa na BBC, alichagua kutumia jina lake la kwanza pekee.

Rae anakumbuka wakati Ajoke akipitiwa na usingizi na kulala kwa muda mrefu, na TB Joshua alikuwa akimfokea na kumnyanyua kwa nguvu kutoka kitandani.

Ajoke anasema baada ya kuteswa kwa miaka mingi, alipoteza hofu yake kwa baba yake akiwa na umri wa miaka 17.

Akikumbuka tukio hilo, Ajoke anasema: "Nilikuwa nikipiga kelele kwa sauti ya juu, na mateso hayakukomea hapo. Yaliendelea kwa muda mrefu sana."

Unyanyasaji kama huo haukuisha, anasema.

"Tunazungumza kuhusu miaka na miaka ya unyanyasaji. Unyanyasaji wa mara kwa mara. Kuwepo kwangu kama mtoto kutoka kwa mama mwingine, kulidhoofisha kila kitu ambacho [TB Joshua] alidai kuwakilisha."

Unyanyasaji huo uliongezeka kwa kiwango tofauti alipokuwa na umri wa miaka 18 hivi, aliamua kumkabili baba yake na kumueleza kuhusu "simulizi za moja kwa moja za watu ambao walifanyiwa unyanyasaji wa kijinsia."

"Niliwaona wanafunzi wa kike wakipanda chumbani kwake. Walikuwa wakienda na kuwepo huko kwa saa nyingi. Nilikuwa nikisikia mambo mengi kuhusu baba yangu huko chumbani akiwa na waasichana, anaongeza Ajoke.

Wanafunzi wa zamani zaidi ya 25, kutoka Uingereza, Nigeria, Marekani, Afrika Kusini, Ghana, Namibia na Ujerumani - ambao walitoa ushuhuda wenye nguvu wa kufanyiwa au kushuhudia unyanyasaji wa kingono.

"Sikuweza kuvumilia zaidi. Niliingia ofisini kwake moja kwa moja siku

Inaendelea Uk 18



Kanisa la Soan

Uchunguzi

TB Joshua aumbuliwa na binti yake

Inatoka Uk. 17

hiyohiyo. Nilipiga kelele kwa sauti kuu: ‘Kwa nini unafanya hivi? Kwa nini unawaumiza wanawake hawa wote?’

“...Nilikuwa nimepoteza kila chembe ya hofu kwa mtu huyu. Alijaribu kuniangalia kwa ukali, lakini nilikuwa nikimtazama machoni,” anasema Ajoke.

Emmanuel, ambaye alikuwa sehemu ya kanisa kwa miaka 21 na alikaa zaidi ya muongo mmoja akiishi katika boma hilo akiwa mfuasi, anakumbuka pia kuanza kuenea kwa tuhuma kutoka kwa baadhi ya wasichana wadogo walioingia chumbani kwa TB Joshua.

Ajoke anasema baada ya kumkabili baba yake, alitolewa ndani ya ofisi yake na kuwekwa katika chumba, mbali na waumini wengine wa kanisa, ambapo alishi katika kifungo kwa zaidi ya mwaka mmoja.

Ni aina ya adhabu ndani ya Scoan inayojulikana kama “adaba”, adhabu ambayo pia binti mwengine, Rae pia alipitia kwa miaka miwili.

Wakati huu Ajoke anasema mara kwa mara alipigwa na mikanda na minyororo.

“Nashangaa jinsi nilivyoishi nyakati hizo. Sikuweza hata kusimama kwa siku kadhaa baada ya vipigo hivi. Sikuweza hata kuoga. Alikuwa akijaribu sana kuwazulia watu kunisikiliza,” anaongeza binti huyo kwa uchungu.

Siku moja Ajoke alipokuwa na umri wa miaka 19, anasema alisindikizwa hadi kwenye lango la mbele ya kanisa na kuachwa hapo. Walinzi wa kanisa, ambao walikuwa na silaha, waliambiwa asiruhusiwe kamwe kurudi ndani. Hii ilikuwa miaka sita kabla ya baba yake kufariki.

“Niliondoka pale, sikujua kwa kwenda, sikujua naenda kuishi wapi. Sikuwa na mtu wa kufikia kwake. Hakuna ambaye angiamini,” anasema.

Akiwa msichana asiye na pesa, Ajoke alifanya alichoweza ili kuishi na aliishi miaka kadhaa mitaani kabla ya kupata



Evelyn ndiye mrithi wa TB Joshua kwa sasa

mwanya wa kwenda uhamishoni.

Aliwasiliana na BBC kwa mara ya kwanza mwaka 2019 baada ya kutazama habari kadhaa za uchunguzi za kipindi cha BBC Africa Eye - hivyo akaona fursa ya kufichua uovu wa baba yake dhidi ya wasichana, na hasa mabinti.

BBC iliwasiliana na Scoan kuhusu madai hayo, lakini kanisa hilo la TB Joshua, likiwa sasa linaongozwa na mkewe, halikujibu.

Kwa msaada wa wanafunzi wa zamani na baadhi ya marafiki wa karibu, hivi karibuni Ajoke aliweza kuondoka mitaani na yuko mafichoni.

“Kila nilipopigwa, kila nilipodhalilishwa, ilinikumbusha tu kwamba kulikuwa na shida kwenye maisha ya baba yangu, lakini pia kwenye mfumo mzima wa kanisa la Scoan,” anaongeza binti huyo.

Wanafunzi wa zamani wameambia BBC kwamba kuona Ajoke akimpinga baba yake kuhusu imani na matendo yake, pamoja na kwamba amekuwa na sifa kubwa, ilikuwa mojawapo ya sababu kuu za kuanza kutilia shaka “mapenzi ya TB Joshua kwa Mungu aliyekuwa akimtaja mara kwa mara kuwa ndiyo nguzo ya uponyaji wake.”


“Hatujui nini kilichokuwa kikitoea, lakini TB Joshua alituweka sote katika utumwa, utumwa kamili wa akili na hatukuelewa nini hasa alichokuwa akitufanya,” anasema Emmanuel.

Kutokana na tuhuma hizi za TB Joshua, vituo vikubwa vya televisheni vilivyokuwa vikishirikiana naye, vimesitisha kurusha vipindi vyote vya kanisa hilo.

Ufunguzi michuano ya soka Afcon



Kila aina ya mbwembwe zilishuhudiwa na dunia katika ufunguzi huo.



Mwanamuziki wa Nigeria, Yemi Alade (kushoto) alipata 'shavu' la kutumbuiza ufunguzi wa mashindano hayo makubwa zaidi Afrika.

Fashfash za kila aina zilishuhudiwa juzi - Jumamosi, Januari 13, wakati wa ufunguzi rasmi wa michuano mikubwa zaidi ya mpira wa miguu Afrika (Afcon). Ufunguzi huo ulifanyika katika Uwanja wa Alassane Ouattara, katika Jiji la Abidjan, Ivory Coast. (Picha zote kutoka mitandao).



'Manjonjo' yalitawala mno katika ufunguzi huo.



Mwezi 'unapokutana' na bahari.



Picha hii iliyopigwa na Evreni Merak Ediyoruz wa Uturuki, inaonesha mwanga wa mwezi unapogonga uso wa bahari na kutengeneza mwonekano wa kuvutia. Picha hii imehotwa kwenye mtandao wa X, haeleswi imepigwa lini na wapi, lakini imependeza gazeti hili kuiweka hapa ili kuwashirikisha wasomaji wake.

GAZETI hili lilianshwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa msunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

